# EE BWANA WEWE UNA FUMBUA MKONO WAKO NA UNATUSHIBISHA

Zaburi 144 B

Musique: Tsongo Basesa Josué (TB-Jos)
PUERI CANTORES CHOEUR SAINT JEAN-PAUL II
PAROISSE SAINT KIZITO/GOMA




1. Bwana ni mwenye huruma na mpole
   mvumilivu na mwingi wa wema
   Bwana ni mwema kwa wote
   huruma yake juu ya kazi zake zote.

2. Macho ya wote yanakutumainia
   nawe unawapa chakula wakati wake.
   Wewe wafumbua mkono wako
   washibisha kwa ukarimu kila aliye mzima.

3. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote
   na mwema katika kazi zake zote.
   Bwana ni karibu na wote wanaomwita
   wote wanaomwita kwa uaminifu.